# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA SHAMBA

**MRUTU AGRO-SOLUTIONS COMPANY LIMITED** ni kampuni binafsi iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania kupitia **BRELA** kwa usajili wa Na. **151143326** ambapo ofisi ipo Morogoro Mjini, Jengo la ushirika, plot na. 20 Zone II ambapo huduma hutolewa popote, ndani na nje ya nchi. Kampuni imesajiliwa kwa malengo ya kutoa huduma mbalimbali ili kuleta '*suluhisho makini*' kwenye changamoto na fursa za Kilimo Biashara, Ufugaji, Uvuvi na Ujasiriamali ili kuongeza kipato kwa mtu mmoja mmoja na nchi kwa ujumla, kupunguza umaskini, kuondoa njaa, kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira, kutumia vizuri fursa na rasilimali zilizopo nchini ikiwemo ardhi inayofaa kwa kilimo kwa ujumla wake, kuboresha afya, lishe pamoja na utunzaji wa mazingira kwa Maendeleo Endelevu ikiwemo utalii wa Kilimo. Huduma kampuni ilizo lenga kutoa ni pamoja na mafunzo ya Kilimo Biashara na Ujasiriamali, Kuandaa maandiko ya miradi, mipango ya kilimo biashara pamoja na vitabu (tayari tumesha andika vitabu mbalimbali vya kilimo biashara na ujasiriamali ikiwemo mazao mbalimbali, ufugaji wa kuku, pamoja na ufugaji wa samaki), Ushauri wa kitaalamu wa Kilimo Biashara (Agribusiness Consultancy), Kupima udongo, Uzalishaji na uuzaji wa miche mbalimbali na mbegu, Ujenzi wa mabwawa ya samaki, Ujenzi wa mifumo ya umwagiliaji, Ujenzi wa vitalu nyumba, Kusindika mazao na kuongeza thamani, Huduma ya usimamizi wa mashamba,/ miradi ya kilimo na ufugaji, Huduma saidizi za kilimo na ufugaji kama vile utoaji wa chanjo za mifugo, kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia, kujenga mabanda ya mifugo, usimamizi wa miradi hiyo pamoja na Huduma za masoko ya bidhaa na mazao mbalimbali ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu.

**Moja ya jambo muhimu sana kwenye miradi ya kilimo na ufugaji linaloweza kusaidia kufanikisha au kutofanikisha mradi ni Usimamizi. Usimamizi mzuri unapelekea mradi kufanikiwa, na usimamizi mbovu unapelekea mradi kushindwa kufanikiwa, mambo mengine yakiwa sawa (*'ceteris peribus conditions'*). Kwa kutambua kwamba kuna watu wanataka kuwekeza kwenye miradi ya kilimo lakini hawana muda wa kusimamia, hawana watu sahihi wa kusimamia, lakini wanataka miradi yao isimamiwe kitaalamu kwa uweledi na ilete tija, sisi kama kampuni tumeliona kama kikwazo au changamoto kwa wadau wetu na tukaja na suluhisho ili kuwasaidia wadau kufikia malengo yao kupitia utoaji wa huduma ya usimamizi wa mashamba (Kupitia trained Shamba boys &**

**shamba girls). Aidha, tunatarajia kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa vijana wa shamba ili miradi inayo anzishwa iwe na wasimamizi wazuri hivyo miradi kuleta matokeo chanya.**

**Katika mfumo huu tulio kuja nao kama kampuni (*Model*) kuna namna mbili za package,**

1. **Tunaratibu zoezi la upatikanaji wa vijana wenye nia, vigezo tulivyoweka, nidhamu, bidii, uadilifu na wenye hofu ya Mungu. Baada ya kuwapata vijana hao, wanapata mafunzo ya Kilimo Biashara mahususi kutokana na miradi wanayoenda kusimamia ili wawe na stadi za ile miradi wanayoenda kufanya kwa nadharia na vitendo kisha kuwaunganisha na miradi husika au kazi husika (hii pia ni njia tunayotumia kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira hasa kwa vijana na kwa watu wenye familia pia). Vijana hao wanaweza kuwa wahitimu wa darasa la saba, kidato cha nne, kidato cha sita na elimu ya juu.Vijana wote wenye taaluma na wasio na taaluma tunashughulika nao, wale watakao pata kuchaguliwa ndio wanaenda kutokana na aina ya mradi ambao mwekezaji anataka. Kama mwekezaji atahitaji tumtafutie kijana wa namna yoyote tunamtafutia na tunampa utaratibu ili apate watu wa kusimamia na kampuni inakuwa inafanya tathmini (*monitoring & evaluation)* mara kwa mara na kutoa ushauri.**
2. **Aidha kuna wawekezaji wengine ambao wanahitaji kusimamiwa na kampuni moja kwa moja kimkataba, huduma hiyo pia inapatikana kwa mawasiliano zaidi wanakaribishwa Mrutu Agro-Solutions Company Limited kupewa utaratibu. Mfumo huu ni kama ule wa Kampuni za Ulinzi.**

✓ ***Kwa sasa kampuni inatafuta vijana waaminifu, wanaojua na wanao penda kufanya kazi, wanaoweza kujisimamia, wenye mtazamo chanya, waaminifu, wavumilivu na wenye nia ya kufanya kazi ambazo watapangiwa. Nafasi hizo ni:-***

1. *Nafasi (1) ya Kijana wa Kiume, mwenye taaluma ya Mifugo, kuhudumia shamba la mifugo kibiashara. Atafanya majukumu yote ya mifugo pamoja na shamba la mazao. Kufanya usafi, kulisha mifugo, utunzaji wa kumbukumbu, kuhudumia mashamba na kuhakikisha mazao bora na mengi yanapatikana kutokana na shamba lililopo. Kituo cha Kazi kipo ndani ya Mkoa wa Kilimanjaro.*
2. *Nafasi (1) ya Kijana wakike, mwenye taaluma ya masuala ya Kilimo na ujuzi wa kilimo cha mbogamboga na matunda. Kazi yake kubwa ni kufanya uzalishaji wa mazao ya mbogamboga na matunda, kuhudumia bustani, kupanda, palizi, kumwagilia mazao,kutunza kumbukumbu, kuvuna mazao na shughuli zingine za usimamizi kwa vibarua wa msimu. Kituo cha Kazi kipo ndani ya Mkoa wa Kilimanjaro.*

3. *Nafasi (1) ya kuhudumia mifugo, kuwalisha, kuwapa chanjo, kuwapa dawa, kuwapa chakula, kufanya usafi, kutunza kumbukumbu na mambo mengine kwa lengo la kufanya mradi ulete faida. Kijana wakike au wa kiume yoyote anaweza kuomba. Kituo cha Kazi ni kati ya Mkoa wa Pwani au Dar es Salaam.*

❖ ***SIFA ZINAZO TAKIWA KWA VIJANA WA SHAMBA KWENYE MIRADI ILIYO TAJWA:-***

1. *Umri miaka 18 hadi 35*
2. *Wawe wachapa kazi wasiwe wavivu na wawe wamepitia mafunzo ya KILIMO KWA NGAZI YA CHETI AU DIPLOMA.*
3. *Wawe na vitambulisho vya NIDA na wasiwe na historia ya kufanya makosa ya jinai (wenye barua za utambulisho kutoka serikali za mitaa husika au sehemu zingine zikiwatambua vizuri ni sifa za ziada).*
4. *Vijana watume ujumbe mfupi wa maneno (Naomba Kazi ya SHAMBA) kwenda kwa namba zifuatazo, 0623299626-Mratibu wa mafunzo kutoka kampuni ya Mrutu Agro-Solutions Company Limited.*
5. *Baada ya kutuma ujumbe mfupi wa maneno, wale watakao kuwa wamechaguliwa watapewa utaratibu mwingine wa kutuma taarifa zitakazo hitajika zaidi kwa kupigiwa simu, taarifa hizo zinaweza kuwa vitambulisho vya NIDA, wasifu wao (CVs), vivuli vya vyeti, barua ya maombi ya kazi ya shamba n,k kulingana na kazi husika.*
6. *Tangazo limetoka leo tarehe 18/01/2023 atakaye tuma ujumbe mapema atapewa kipaumbele pamoja na wale walio pitia mafunzo maalumu ya ziada na uzoefu wa kazi husika.*
7. *Aidha, watakao chaguliwa watapatiwa mafunzo ya muda mfupi kabla ya kuanza kazi.*